



Siku ya “Karibu Kingston”

Tarehe 27 Oktoba, 2024 ni siku ya kuwakaribisha watu wote ambao ni wageni Kingston. Wageni wanaweza kuwa walitoka sehemu nyengine nchini au pia watu walitoka nchi yoyote ile duniani.





WELCOME TO KINGSTON DAY

Kingston inakusudia kuwa jamii inayokaribisha na kujumuisha watu wote; na

Mji wetu unazidi kuwa na watu aina tofauti tofauti, watu kutoka nchi mbalimbali na maeneo mbalimbali nchini wanaoita Kingston nyumbani kwao; na

Michango ya watu ambaeo ni wapya katika jamii inachangia kuimarishe ustawi wa kiuchumi, uchangamfu wa jamii, na utamaduni wa Kingston; na

Kingston inazidi kujitolea kuhakikisha kuwa wageni wakiwasili wanahisi kuwa wamekaribishwa na wanaweza kupata msaada na huduma mbalimbali; na

Serikali ya Jiji la Kingston ikishirikiana na Kingston Immigration Partnership (KIP) na mashirika mengine ya kutoa huduma tofauti, wameandaa Siku ya Kuwakaribisha Wageni Kingston itakayofanyika tarehe 27 Oktoba, 2024.

Kwa hiyo, mimi, Meya Brian Paterson, kwa niaba ya Baraza la Jiji la Kingston, ninatangaza kuwa tarehe 27 Oktoba, 2024 ni "Siku ya Kuwakaribisha Wageni Kingston".

Bryan Paterson
Meya

Zawadi ya Kukukaribisha Kingston

Ikiwa wewe ni mgeni Kanada, unaweza kupata vocha ya bure ya kukukaribisha nchini iliyodhaminiwa na serikali ya Jiji la Kingston katika ofisi zifuatazo:

- **Immigrant Services Kingston and Area (ISKA)**
iliyoko 837 Princess Street, #201
- Ofisi ya **KEYS** iliyoko 255 Bagot Street, Unit C
- Ofisi ya **ACFOMI** iliyoko Barriefield Centre, 760 Highway 15

Ikiwa wewe ni mwanajeshi na familia yako imehamishwa Kingston, utapa zawadi ya kuwakaribisha Kingston katika ofisi ifuatayo:

- **Kingston Military Family Resource Centre**
iliyoko 32 Lundy's Lane

Zawadi hii itakuwezesha upate kutumia vitu tofauti mjini kwa mfano: kadi ya kutumia basi, kadi ya kuingia kwenye ukumbi wa mazoezi na michezo, vocha ya kuangalia michezo ya kuigiza pale Grand Theatre, pamoja na vocha za kuzuru makavazi.





Programu ya Manispaa ya kutoa Msaada wa Kulipa Ada

Programu ya Manispaa ya kutoa Msaada wa kulipa Ada unawasaidia watu wenyewe kipato cha chini waweze kulipa ada mbali mbali kama:

- kadi ya kutumia basi ya bei nafuu
- Huduma za afya za ziada
- Umiliki bora wa wanyama
- Burudani kwa bei nafuu
- Programu ya usafiri kwa watu walioajiriwa
- Grand OnSTAGE
- Ziara ya makavazi ya Pumphouse

Msaada unatolewa kwa wale watakaotuma maombi yao kwanza. Msaada unapatikana hadi fedha zote zilizotengewa mwaka huo kuisha.

Ili kutuma ombi, tengeneza akaunti kwenye tovuti ya mykingston.ca au tembelea ofisi ya Huduma za Kijamii na Makazi iliyoko 362 Montreal Street.



Piga Scan hapa ili
utengeneze
akaunti ya
mykingston.ca.

Huduma za Watoto

Kingston ina bodi nne za shule : bodi mbili za Kiingereza na mbili za Kifaransa :

- **Limestone District School Board** (LDSB) ni Bodii ya Shule za Umma za lugha ya Kiingereza
- **Algonquin & Lakeshore Catholic District School Board** (ALCDSB) ni Bodii ya Shule za Kikatoliki za lugha ya Kiingereza
- **Conseil des écoles publics de l'Est de l'Ontario** (CEPEO) ni Bodii ya Shule za Umma za lugha ya Kifaransa
- **Conseil des écoles catholiques du Centre-Est** (CECCE) ni Bodii ya Shule za Kikatoliki za lugha ya Kifaransa

Serikali ya Jiji la Kingston imetengeza orodha kwenye mtandao ya wazazi wenye watoto wadogo wanaotafuta huduma za watoto. Pia kuna Vituo vya Watoto na Familia vya EarlyOn vinavyotoa msaada wa bure kwa familia zenye watoto wenye umri wa miaka 0 hadi 6.



Scan hapa ujifunze zaidi
kuhusu bodi za shule mjini Kingston



Scan hapa ujifunze zaidi
kuhusu huduma za watoto,
msaada ya kifedha na
programu za watoto





Burudani, Matukio, na Vitu vya kufanya

Kingston ina programu za aina nyingi na vitu mbalimbali vya kufanya kwa kila mtu, iwe unavutiwa na programu maalum, burudani ya bei nafuu, michezo, sanaa, mazoezi, afya, ustawi, au kujitolea.

Scan hapa ujifunze zaidi kuhusu
vitu vya kufanya na matukio ya
Kingston.



Kwa maelezo zaidi kuhusu huduma za hapa mjini kama vile Kingston Transit au huduma za takataka, tembelea cityofkingston.ca.

Huduma za Afya

Ikiwa unahitaji huduma za matibabu, tembelea:

- **Emergency Department** iliyoko 41 King Street West. Hii ni hospitali ya matibabu ya dharura
- **Urgent Care Centre** iliyoko 166 Brock. Hii ni kliniki ya kutoa matibabu yasiyo ya dharura. Utaenda hapa ikiwa unahitaji kumuona daktari lakini hauna darura kama vile majeraha au ugonjwa uliozidi
- **Children's Outpatient Clinic** iliyoko 166 Brock Street. Hii ni Hospitali ya Watoto. Inatoa huduma za afya za haraka kwa watoto walio na umri wa miaka 18 au chini

Kwa ushauri wa afya wa bure na wa siri kutoka kwa nesi wa **Health811**, piga simu nambari 811. Huduma hii inapatikana kwa lugha nyingi tofauti.

Ikiwa unahitaji mtu wa kukupa huduma za afya za mara kwa mara kama vile daktari wako wa familia, jiandikishe na **Health Care Connect** kwenye mtandao au kwa kupiga simu 811.



Scan hapa ili
ujiardikishe na
**Health Care
Connect.**





Msaada wa Chakula

Kuna sehemu mbalimbali Kingston za kupata chakula bora kwa bei nafuu kwa mfano: masoko ya wakulima, vibanda vya mboga, na sehemu za kutoa msaada wa chakula.



Scan hapa
upate
orodha ya
kina zaidi.



Scan hapa
upate
orodha ya
vyakula aina
mbalimbali.

Sehemu za kupata msaada wa chakula:

1. **Partners in Mission Food Bank** iliyoko 140 Hickson Avenue
2. **Salvation Army** iliyoko 342 Patrick Street
3. **St. Vincent de Paul Society** iliyoko 85 Stephen Street
4. **Martha's Table** iliyoko 629 Princess Street
5. **Cafe Church** iliyoko 333 Princess Street, #200
6. **St. Mary's Drop-In** iliyoko 260 Brock Street
7. **Lunch by George** iliyoko 129 Wellington Street

Huduma za Ajira

Je, unatafuta kazi au msaada wa kujijenga kikazi?

Watu wengi wanastahiki kupata huduma za ajira, mafunzo na ushauri wa **bure**. Mifano ya huduma hizi ni: kujenga wasifu, kutafuta kazi na kupata mafunzo ya kuongeza ujuzi wa kikazi. Huduma hizi zinapatikana katika mashirika yafuatayo:

- **ACFOMI** kwa msaada wa lugha mbili (Kifaransa na Kiingereza) iliyoko Barriefield Centre, 760 Highway 15
- **KEYS** iliyoko 182 Sydenham Street
- **ReStart** iliyoko 900 Montreal Street
- **Huduma za Ajira za Chuo cha St. Lawrence** iliyoko 785 Midpark Drive, #101
- **March of Dimes** kwa watu wenye ulemavu iliyoko 920 Princess Street, #360

Ikiwa wewe ni mwanafunzi wa elimu ya juu wa kimataifa, wasiliana na ofisi ya huduma za kazi katika shule yako ili upate msaada maalum.





Huduma za Kupambana na Chuki zilizoko Kingston

Jiji la Kingston linajitahidi kujenga jamii ambayo kila mtu anaweza kuishi kwa salama, afya njema, na ahisi kuwa anakaribishwa.

Changamoto moja ya kutimiza ahadi hiyo ni kuenea kwa chuki. Madhumuni ya matendo ya chuki ni kuwafanya wale walioathirika wajisikie kuwa hawana usalama.

Ikiwa unahisi umefanyiwa uhalifu uliosababishwa na chuki, unaweza kuripoti kwa polisi kwa kutumia QR code iliyoko hapa chirini au kwa kupiga simu:

- 911 ikiwa ni dharura - maisha yako yako hatarini
- 613-549-4660 ikiwa si dharura



Scan hapa ili upige
ripoto kwa Polisi wa
Kingston mtandaoni



Scan hapa ili ujifunze zaidi
kuhusu huduma nyingine
na njia za kuripoti.



Asante kwa washirika wote!



Immigrant Services Kingston and Area
A part of Kingston Community Health Centres (KCHC)



Welcome to Kingston App

Are you new to Kingston?

Discover the Welcome to Kingston App, your guide to your new community.

Key Features:

- Find essential local resources, from healthcare to housing.
- Connect with community organizations ready to assist you.
- Stay informed about cultural events, festivals, and activities.
- Access support in over 15 languages

DOWNLOAD BELOW

